

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 022 2126826
Nukushi: 022 2126834
Tovuti: www.habari.go.tz
Baruapepe: km@habari.go.tz



S. L. P 25,
Mtaa wa Habari,
Mji wa Serikali Mtumba,
40481 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

SALAMU ZA POLE

Februari 24, 2021 - Dodoma

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa (Mb) amepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Mwanamuziki wa Dansi Waziri Sonyo kilichotokea Februari 23, 2021 Kibaha Mkoa wa Pwani.

“Hili ni pigo katika sekta ya Sanaa kwa ujumla kwa kuondokewa na mmoja ya wasanii waliochangia kukuza tasnia ya muziki wa dansi nchini ambao ni miongoni mwa mtindo wa muziki unapendwa sana,” alisema Bashungwa.

Marehemu Sonyo alianza safari yake ya muziki Handeni na Hale mkoani Tanga akiwa na bendi ya SOT Sound na atakumbukwa kwa wimbo wa “Masimango” aliouimba kwa umahiri alipokuwa na Bendi ya TOT Plus. Pia alifanyakazi ya muziki akiwa na bendi za Super Melody na Sky Melody za Dodoma, Bambino Sound, Chuchu Sound, African Ocean, Mwenge Jazz, Victoria Sound pamoja na Bendi ya Kiteshi yenye maskani yake Kibaha mkoa wa Pwani.

Waziri Bashungwa ametoa pole kwa familia, Chama cha Muziki wa Dansi Tanzania (CHAMUDATA), wasanii, wadau wote wa tasnia ya sanaa, ndugu, jamaa, na marafiki. Pia anawaomba wote kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema, wapate nguvu, ujasiri na moyo wa ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu.

Imetolewa na

Eleuteri E. Mangi

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.**